
# WANAWAKE na ARDHI

Ardhi ni Uhai

HAKIARDHI

TOLEO LA 2 DESEMBA 2018



Na; Fadhili D. Sengele

## TAMATI YA DHULUMA YA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE WA KATA YA MLOWA, IRINGA

Dhuluma inaweza kutafsiriwa kuwa kupora, kulaghai, au kuchukua bila ridhaa au bila kufahamu kama unachukuliwa kilicho chako. Katika nchi za Kiafrika, Tanzania ikiwa ni mojawapo wanawake wamekuwa wakidhulumika haki zao katika ardhi zinazofanywa na wana familia au jamii inayomzunguka. Wanawake wamekuwa wakipokonywa haki zao kwa makusudi au kwa kutokujua na wengine wanafanyiwa dhuluma kutokana na mfumo dume uliotamalaki katika makabila mengi ya Kiafrika. Taasisi ya ICISO ambayo kwa ufadhili wa Shirika la *Foundation for Civil Society* wamejikita katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili wanawake katika sekta ya ardhi hasa katika maeneo

*Inaendelea uk. 4*

## NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

**YALIYOMO**


- TAMATI YA DHULUMA YA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE WA KATA YA MLOWA, IRINGA — 1 & 4
- MSAADA WA KISHERIA WANUSURU ARDHI YA MAMA MJANE KIJIJI CHA NYARUTANGA, MOROGORO — 5-6
- ELIMU YA HAKI ZA ARDHI IANZIE SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI — 6
- WANAUME WA KIMAASAI NDIO WATETEZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE WILAYANI KITETO — 8
- HAKI ZA ARDHI NI MSINGI WA MAENDELEO KWA WANAWAKE NA JAMII — 12
- UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA ARDHI NI KUFAHAMU HAKI NA WAJIBU WAKE — 14

# TAHARIRI

## UTANGULIZI



Cathbert Tomitho

# WANAWAKE&ARDHI

*Nafasi Ya Sheria Za Ardhi Katika Kulinda Haki Za Wanawake*

Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinasisitiza juu ya haki sawa kwa mwanaume na mwanamke katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi kama sehemu ya mali ambayo kila raia wa Tanzania ana haki ya kumiliki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake.

Pamoja na kuwa Sera na Sheria za ardhi kutambua usawa katika umiliki wa ardhi bado tafiti zinaonesha kuwa wanawake hasa waliopo vijijini wanakumbana na unyanyasaji mkubwa kutokana na mila na desturi ambazo hazimpi nafasi kama anayopata mwanaume.

Kumekuwepo na kesi kadha wa kadha zikiwahusisha watoto wa kike waliokosa urithi wa ardhi kutoka kwa wazazi wao kwa sababu tu wao ni waolewaji kwahiyo ardhi ipo kwa waume zao. Halikadhalika tumeshuhudia kesi nyingine za wanawake wakinyanyaswa pindi waume zao wanapofariki hivyo kukosa haki ya kumiliki ardhi na nyumba walizochuma na waume zao wakati wa ndoa yao.

Kutokana na vitendo hivi kuendelea Shirika la Foundation for Civil Society linafadhili mradi wa kutetea haki za wanawake katika ardhi kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini ikiwa ni pamoja na Pwani, Morogoro, Iringa, Singida, Manyara na Arusha. Mradi huu unatekelezwa na mashirika ya ngazi ya wilaya yaliyopo katika maeneo haya kwa kushirikiana na Taasisi ya HAKIARDHI.

Jarida hili linajumuisha matokeo ya utekelezaji wa mradi huu katika maeneo haya kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii na wadau wengine wanajifunza matokeo chanya pamoja na changamoto zinazowakabili wanawake. Kwa kusoma jarida hili utajifunza uzoefu kutoka maeneo mengine ambao ni muhimu sana katika kutetea haki za ardhi kwa wanawake.

*Heri ya Mwaka Mpya 2019.*

*Cathbert Tomitho*
***Mhariri***



Na; Fadhili D. Sengele

# UMILIKI WA ARDHI KIMILA NI UMILIKI HALALI KWA MUJIBU WA SHERIA ZA ARDHI



*Baadhi ya wanawake wa kijiji cha Irindi waliopatiwa vyeti vya hakimiliki ya kimila.*

Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinatambua aina mbili kuu za umiliki wa ardhi nchini, ambazo ni umiliki wa hati na umiliki wa kimila. Umiliki wa hati unatumika zaidi katika ardhi za kundi la ardhi ya jumla wakati umiliki wa kimila unatumika kwenye kundi la ardhi ya kijiji. Kwa mujibu wa Sheria hizi mbili umiliki wa aina zote mbili una nguvu sawa katika macho ya sheria.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 mtu, kundi la watu na taasisi inayotaka kumiliki ardhi kwenye ardhi ya kijiji anaweza kupata Cheti cha Hakimiliki ya Kimila. Hiki ni cheti kinachotolewa na Halmashauri ya Kijiji kwa mujibu wa fungu la 25 la Sheria ya Ardhi ya Vijiji ili kutambua au kuthibitisha umiliki wa ardhi wa mwombaji kwa taratibu za kimila.

Kuna nadharia nyingi sana zinazosukuma watu kutaka kupata Cheti cha umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutambulika kama mmiliki halali kisheria, kupata mkopo kutoka taasisi za kifedha pamoja na kuitumia kama dhamana kwenye mahitaji mbalimbali ya kijamii kama vile kwenye kesi.

*Inaendelea uk. 4*

›› Inatoka uk. 1

ya vijijini. Mnamo mwezi Agosti, 2018 Taasisi ya ICISO ilifanya mafunzo ya haki sawa katika umiliki wa ardhi na rasilimali nyinginezo sambamba na mafunzo hayo ICISO imetekeleza kazi mbalimbali zilizolenga kuleta usawa katika jamii. Jitihada hizi zimepelekea mabadiliko mbalimbali ikiwemo kurudishwa ardhi walizodhulumiwa wanawake.

Kwa mfano Bi. Neema Mgina mkazi wa kijiji cha Mafuluto kata ya Mlowa wilaya ya Iringa, aliolewa na Antoni Metelii mwaka 2007 na kubahatika kupata watoto wanne. Katika kipindi cha ndoa yao walifanikiwa kuchuma mali kadha wa kadha ikiwa ni pamoja na mashamba na pikipiki. Mwaka 2017 Bw. Antoni aliamua kumuacha Bi. Neema na kuoa mke mwingine. Bi. Neema alipoachika hakupata mgao wowote wa mali walizochuma. Hali hii ilimfanya aishi maisha ya shida na taabu nyingi sana. Akisimulia kwa uchungu Bi. Neema alisema. *"Mume wangu alipomuoa huyo mwanamke anayeishi naye sasa kata ya Pawaga alichukua pikipiki tuliyonunua kwa nguvu zetu na kumpa Mke mdogo. Pikipiki hii ilikuwa ikitusaidia kujipatia fedha kwa matumizi na mahitaji ya nyumbani. Vilevile aliuza shamba la familia lenye ukubwa wa ekari 20 pasipo kunishirikisha. Hivyo ni mwaka umepita sasa sina shamba la kulima kwaajili ya kujipatia chakula na watoto wangu wakati yeye hanisaidii chochote."*

Bi. Neema aliendelea kueleza kuwa;

*"Mwezi wa nane mwaka 2018 Taasisi ya ICISO walifanya mafunzo ya haki za ardhi ambapo nilibaini kuwa naweza kupata haki yangu kwa kwenda serikali ya kijiji. Baada ya mafunzo nilienda kwa Mwenyekiti wa kitongoji kumueleza tatizo langu lakini majibu aliyonipa ni kuwa mwanaume ndiye mwenye maamuzi ya mwisho kwenye familia yake kwahiyo mume wangu anayofanya ni sahihi kwasababu mashamba na mali nyingine zote ni za kwake. Baada ya kuona Mwenyekiti wa Kitongoji ameshindwa kuisimamia haki yangu niliamua kuwaeleza maafisa wa ICISO ili nao wanisaidie kupata haki yangu."*

Baada ya Maafisa wa ICISO kumsikiliza Bi. Neema na kufuatilia kisa hiki waliamua kulipeleka kwenye chombo cha utatuzi wa migogoro ya ardhi ambacho ni Baraza la Ardhi la Kijiji cha Mafuluto ambalo wajumbe wake walishapatiwa mafunzo ya Sheria za Ardhi.

Kesi hiyo ilisikilizwa kwa miezi mitatu ambapo tarehe 26 Novemba, 2018 Baraza la Ardhi la Kijiji lilitoa uamuzi kuwa Bi. Neema arudishiwe ekari 10 kati ya zile 20 zilizouzwa na aliyekuwa mume wake kwakuwa Baraza lilibaini kuwa maamuzi ya kuuza shamba yalifanyika kwa nia ya kumkomoa Bi. Neema. Baada ya maamuzi ya Baraza pande zote mbili zilizridhia na kusaini maridhiano hayo mbele ya Mwenyekiti wa Baraza na mashahidi.

Mfano huu wa Bi. Neema na mume wake unatupa picha kubwa ya jinsi wanawake wanavyonyanyaswa na wanaume kwa kutokujua haki zao kwa mujibu wa Sheria za Ardhi na Sheria nyinginezo. Lakini pale wanawake wanapokuwa na uelewa wa haki na wajibu wao basi ni rahisi wao kulinda haki zao na watoto wao.

›› Inatoka uk. 3

Kabla ya ujio wa Sheria za Ardhi mwaka 1999 haikuwa rahisi kwa wazalishaji wadogowadogo vijijini kuwa na uhakika wa kumiliki ardhi kwa kupata hakimiliki. Hali ilikuwa mbaya zaidi kwa wanawake ambao walinyanyaswa zaidi kutokana na mila na desturi kuwakandamiza kupata haki hiyo ya umiliki.

Kwa kutambua changamoto zinazowakabili wanawake kwenye umiliki wa ardhi, Taasisi ya ICISO chini ya ufadhili wa Shirika la Foundation for Civil Society walifanya mafunzo kuanzia mwaka 2017 juu ya umuhimu wa kuwa na cheti cha umiliki wa ardhi.

Sambamba na kuhimiza watu kuomba hatimiliki wananchi walielezwa madhara ya hati hizo kama hazitotumika vyema ikiwa ni pamoja na mashamba yao kuuzwa endapo watayaweka rehani wakati wa kukopa na kushindwa kurejesha.

Kutokana na elimu kuwa na hamasa kubwa kwa wananchi walio wengi pamoja na viongozi wa vijiji mpaka kufikia mwezi Oktoba 2018 wanawake wapatao arobaini (40) na mwanaume mmoja (1) kutoka vijiji vya Irindi, Magana na Mahenge vilivyopo wilaya ya Kilolo walifanikiwa kupata hatimiliki za kimila. Pamoja na kuhamasisha na kutoa mafunzo ICISO walichukua jukumu la kuwasaidia wanawake hao kufuatilia hatimiliki zao katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya.

Taasisi inaendelea kuhamasisha wanawake na wanavijiji wote kwa ujumla waweze kutambua umuhimu wa kumiliki na kutumia ardhi kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa chakula na bidhaa nyingine. Ikiwa ni pamoja na kupunguza migogoro ya ardhi inayotokea kwenye vijiji kutokana na kukosekana na utaratibu sahihi wa upangaji wa matumizi ya ardhi na mgawanyo wa rasilimali zilizopo katika vijiji kwa makundi yote ya watumiaji wa ardhi.



Na; Peter Kimath

# MSAADA WA KISHERIA WANUSURU ARDHI YA MAMA MJANE KIJIJI CHA NYARUTANGA, MOROGORO



*Bi. Fatuma Mpeza akitoa ushuhuda jinsi alivyonyanyasika katika kudai haki ya kumiliki mali.*

Mila na desturi za makabila mengi nchini Tanzania ni mila zilizo kandamizi dhidi ya wasichana na wanawake hasa katika kupata na kumiliki rasilimali ardhi na mali nyinginezo ikiwa ni pamoja na nyumba. Mkoa wa Morogoro ni moja ya mikoa yenye makabila ambayo mila zake zinawanyanyasa wanawake. Kwa kutambua hali hii taasisi ya Morogoro Para Legal Center (MPLC) kupitia ufadhili wa Shirika la *Foundation for Civil Society* inatakeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake ambao ndani yake unajumuisha utoaji wa msaada wa kisheria bure kwa wanawake na wananchi kwa ujumla ambao kwa namna moja au nyingine wanapoteza haki zao kwa kutokufahamu haki na wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Kisa cha Bi. Fatuma Mpeza mkazi wa Kijiji cha Nyarutanga, Wilaya ya Morogoro kinadhihirisha nafasi ya msaada wa kisheria katika kuwakomboa wanawake hasa waishio vijijini katika kupata haki zao za ardhi.

Bi. Fatuma alifiwa na mume wake Novemba 2016 ambaye alizaa naye watoto 2 wa kike ambao ni Jackline Denis mwenye miaka 11 na Josephine Denis mwenye miaka 7, Jackline anasoma darasa la sita shule ya msingi Milengelengwe wakati Josephine anasoma shule ya awali.

Baada ya kumaliza msiba wa mume wake, Bi. Fatuma alianza kupokea maneno ya kejeli na vitisho kutoka kwa ndugu wa marehemu mumewe. Wengine walidiriki kumwambia kuwa hana mamlaka wa haki ya kumiliki mali yoyote aliyoacha marehemu ndugu yao kwasababu yeye ameolewa tu kwahiyo ni wa kuja na aliyemleta amekwisha kufariki. Walifikia hatua kumwmabia pia kuwa hawezi kupata chochote na hakuna mtoto mwenye haki ya kupata urithi kwa sababu kwa mila zao watoto wa kike hawana haki ya kurithi mali kwakuwa wataolewa.

Bi. Fatuma alilazimika kurudi nyumbani kwa wazazi wake ambako ni kijiji cha jirani cha Milengwelengwe baada ya manyanyaso ya wakwe zake kuzidi. Bi Fatuma anasema kuwa,

> *"Kusema kweli nilikosa Amani kwasababu hakuna aliyekuwa ananitetea, niliishi katika hali ya mateso na watoto wangu."*

Wakati Bi. Fatuma akiendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo lililokuwa linamkabili alikutana na Mhamasishaji wa Masuala ya Ardhi Bi. Shani Mkanga ambaye amepata mafunzo kutoka MPLC na kuamua kumpeleka katika kituo cha Wasadizi wa Kisheria katika Kata ya Mngazi.


Walipofika ofisi za Mngazi, Baba Mkwe wa Bi. Fatuma aliandikiwa barua ya wito wa kwenda kusikiliza madai ya mkwe wake. Baba Mkwe alitii wito na kufika ambapo kila mmoja alieleza hali halisi ilivyo. Baada ya mazungumzo hayo wote wawili walipewa somo la haki za ardhi kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za mwaka 1999 ikiwa ni pamoja na haki za wanawake katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi ikiwa ni pamoja na wanawake kupata, kurithi, kupewa, kununua, kuuza na kugawa ardhi kama mwanaume alivyo na haki hizo.

Pamoja na majadiliano ya muda mrefu bado Baba Mkwe alikataa Bi. Fatuma apewe haki ya

kusimamia na kumiliki mashamba na nyumba walizochuma na marehemu mume wake. Hali hiyo ilisababisha Wasadizi wa Kisheria kumwongoza Bi. Fatuma kwenda mahakamani, ambapo mahakama iliamua kuziita familia za pande zote mbili.

Shauri lilisikilizwa muda mrefu ambapo Mahakama iliwaamuru ndugu wa mume kutokumnyanysa Mjane huyo. Vilevile Mahakama iliamua kuwa mrithi halali wa mali za marehemu ni Mjane na watoto wake. Mahakama pia iliamuru mjane Fatuma kupewa nyumba waliokuwa wanajenga na mumewe, kitanda, kabati, na vyombo vyote vya ndani ili aweze kuendelea kulea watoto wake.

> *Baada ya Mahakama kutoa maamuzi hayo, Bi. Fatuma alisema maneno yafuatayo; "Nawashukuru sana wasaidizi wa kisheria wa Kituo cha Mngazi kwa mwongozo na msaada walionipa mpaka nikafanikiwa kupata haki yangu. Naahidi kusimamia vizuri mali nilizochuma na marehemu mume wangu ikiwa ni pamoja na kumalizia nyumba tuliyokuwa tukijenga kabla hajafariki ili watoto wetu waishi maisha mazuri na mimi kuendeleza shughuli za uzalishaji mali kupitia kilimo na biashara.*



*Na Happiness Mfinanga*

# ELIMU YA HAKI ZA ARDHI IANZIE SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Kwa muda mrefu kumekuwa na dhana kuwa wanaostahili kupata elimu na mafunzo juu ya Sheria za Ardhi na haki za ardhi kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanawake, wakulima na wafugaji ni watu wazima na viongozi tu katika ngazi mbalimbali. Ndio maana ni nadra sana kwa taasisi za umma na asasi za kiraia kutoa elimu hii kwa watoto wa shule za misingi na sekondari. Pasipo kufahamu kuwa baada ya miaka kadhaa wanafunzi walioko katika shule hizi ndio watakuwa watumiaji wa ardhi na hata viongozi katika ngazi mbalimbali nchini.

Kwa kutambua mapungufu hayo taasisi ya TAWLA kupitia ufadhili wa shirika la *Foundation for Civil Society* kupitia mradi wa haki za ardhi kwa wanawake wameamua kuanzisha klabu za kujisomea masuala ya ardhi kwa wanafunzi wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Tangu kuanzishwa kwa klabu hizo Januari 2018 wanafunzi wanachama wamekuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya haki za ardhi tofauti na ilivyotarajiwa. Wamekuwa wako haraka sana katika kujisomea vitabu vya masuala ya haki za ardhi na kuwa na mijadala ya kujadiliana kile ambacho wamekielewa kutoka katika vitabu mbalimbali. Wanafunzo hawa wamejipangia kukutana mara moja kwa wiki kwa lengo la kusoma na kujadiliana.

Baadhi ya wanafunzi katika klabu hizi wamekuwa na msaada mkubwa katika familia zao na jamii kwa ujumla. Kwa mfano mwanafunzi aitwaye Anitha Kaaya kutoka Shule ya Sekondari Nkoarisambu amekuwa akitetea haki ya Shangazi yake kupata ardhi kama Baba yake. Anitha anasema;

> *Baada ya kusoma na kuelewa haki za wanawake na wasichana katika ardhi, nilikwenda kumuuliza Babu yangu kuwa ni kwanini hakumgawia shamba Shangazi yake kama alivyofanya kwa Baba yake ambaye ni kaka wa shangazi.*

Anitha ni mfano tu wa wanafunzi wengi ambao wameanza kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii wanazoishi kwa kutoa elimu kwa wazazi, ndugu na majirani zao kuhusu haki za ardhi. Wanafunzi wamekuwa ni wadadisi kwenye mambo yanayoendelea katika vijiji vyao pamoja na uwezo kuchambua na kuunganisha matukio katika maisha halisi na kile wanachojifunza darasani. Baadhi ya wanafunzi hawa wameweka malengo ya kusoma masomo ya sheria watakapofika Vyuo Vikuu ili kuja kuwasaidia wanawake, watoto na wanajamii wote wanaonyanyasika kwa kutokufahamu haki zao kwa mujibu wa sheria mbalimbali.





Na Jackson Estomih Muro

# FAMILIA ILIYODHULUMIWA SHAMBA MWAKA 1966 YAREJESHEWA MWAKA 2018 HUKO MERU

Kukosekana kwa elimu ya Sheria za Ardhi kenye maeneo mengi nchini hasa ya vijijini kumekuwa ndio chanzo cha migogoro ya ardhi hasa kutokana na watu wengi kujipatia ardhi kwa njia ambazo sio halali kwa mujibu wa Sheria. Pamoja na kuwa Sheria za Ardhi za mwaka 1999 zinaainisha njia mbalimbali za upatikanaji wa ardhi ambazo ni kurithi, kupewa na serikali, kununua na kupewa zawadi. Upatikanaji wa ardhi kwa njia ya kufyeka pori ambao ulitumika miaka ya nyuma ulifutwa na Sheria za Ardhi za mwaka 1999.

Taasisi ya CEDESOTA kupitia ufadhili wa Shirika la Foundation for Civil Society inatekeleza mradi wa kuwajengea uwezo wanawake na wananchi kwa ujumla kutambua haki zao za ardhi kwa mujibu wa sheria katika Wilaya ya Meru. Kwa mwaka 2017 taasisi ilitoa elimu kwa wanawake zaidi ya thelathini (30). Kupitia elimu hii wanawake hawa wamepata haki zao za ardhi pamoja na kuwasaidia wengine ambao hawakupata nafasi ya kushiriki katika mafunzo hayo.

Mojawapo ya mafanikio ya mradi huu ni mafunzo yaliyotolewa kwa kumshirikisha Bi. Kesia Kaaya ambaye ni Mwenyekiti Msaidizi wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Makiba. Baada ya mafunzo Bi. Kesia alifanikiwa kumsaidia Bi. Zuhura Haji kufuatilia ardhi ya familia yao ambayo iligawiwa pasipo utaratibu na Baba yao mwaka 1966. Kwa mujibu wa Bi. Zuhura ambaye alinukuliwa akisema mwaka 1966 baba yake mzazi aligawa ardhi kiholela kwa Ndugu Mrema pasipo kuandikishana. Baada ya elimu kutoka Cedesota alipata mwongozo wa Bi. Kesia wa kudai mali za baba yake lakini aligonga mwamba kwani mila na desturi hazikutoa mwanya kwa mtoto wa kike kufuatilia mali za Baba yake.

Ilipofika mwaka 2018 Bi. Zuhura alirudi kwa Bi. Kesia kwa lengo la kupata msaada na elimu zaidi jinsi gani anaweza kurejesha mali alizodhulumiwa mzazi wake. Bi. Kesia alimshauri Bi. Zuhura apelike malalamiko yake kwenye Ofisi ya Serikali ya Kijiji.

Baada ya kuwasilisha ofisi ya kijiji, Mwenyekiti wa kijiji alitoa wito wa mlalamikiwa Ndugu Mrema kufika ofisi ya Kijiji kuthibitisha uhalali wake katika kutumia na kumiliki ardhi ya Mzee Haji, baba yake Bi. Zuhura. Katika usikilizaji wa shauri hilo ilibainika kuwa mlalamikiwa hakuwa na uhalali wowote wa maandishi au makubaliano yoyote ya kisheria ya kutumia na kumiliki ardhi yenye mgogoro. Hivyo uongozi wa kijiji uliamua kuwa mlalamikiwa arudishe ardhi hiyo kwa mlalamikaji ambaye ni mtoto wa kike wa Mzee Haji.

Bi. Zuhura alikabidhiwa shamba hilo lenye ukubwa wa ekari moja mwezi Juni 2018 na anaendelea kulitumia hadi sasa. Bi Zuhura alieleza kuwa amejawa na amani na furaha kwa sababu familia imepata eneo ambalo inalitumia kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile mahindi, ndizi, maharagwe na mbogamboga kwajili ya matumizi ya nyumbani na ziada kwa biashara.

B. Zuhura kwa maneno yake mwenyewe anakiri kuwa;

> *“Isingekuwa ni elimu niliyoipata kuhusu Sheria za Ardhi nisingeweza kuikomboa ardhi tuliyodhulumiwa. Nashauri elimu hii itolewe kwa watu wengi zaidi kwasababu hawajui Sheria inasemaje kuhusu haki zao.”*



*Bi. Zuhura Haji akiwa katika shamba alilorudishiwa na uongozi wa kijiji baada ya familia yake kudhulumiwa kwa muda mrefu.*



Na Lilian Cuthbert Mono

# WANAUME WA KIMAASAI NDIO WATETEZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE WILAYANI KITETO

Kifungu cha 3(2) cha Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 kinaainisha ya kwamba haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia na kuuza au kuigawa ardhi ifahamike kuwa ni sawa sawa na haki ya mwanaume yoyote kwa viwango vilevile na masharti yale yale. Kifungu hiki hakieleweki sana katika jamii nyingi za Tanzania na hasa katika jamii ya wafugaji wa Kimaasai ambayo haiamini kuwa mwanamke anaweza kumiliki ardhi.

Kutokana na changamoto zinazowakumba wanawake katika kumiliki ardhi katika jamii ya Wamaasai katika Wilaya ya Kiteto, Manyara. Taasisi ya Ujamaa Community Resource Team (UCRT) kwa ufadhili wa Shirika la *Foundation for Civil Society* linatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake. Katika mradi huu kuna mafunzo ya Sheria za Ardhi kwa viongozi wa vijiji, wa kimila na wanaume. Pia kuna mafunzo ya kuwajengea uwezo Mabaraza ya Wanawake.

Miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo ni Ndugu Yakobo Olisiaji ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Orkitikiti. Ndugu Yakobo ana wake wawili ambao ni Bi. Maria na Bi. Paayai. Bi. Paayai ambaye ni mke mdogo, yeye ni mjumbe katika Baraza la Wanawake la Kijiji ambapo baada ya mafunzo kwenye Baraza hakusita kumshirikisha mke mwenza Bi. Mary kuhusu nafasi ya mwanamke katika kupata na kumiliki ardhi.


Bi. Maria alichukua uamuzi wa kuomba ardhi kutoka kwa mume wake Ndugu Yakobo kwa kumuelea wazi mumewe kuwa kwa kuwamilikisha wake zake ardhi kutasaidia ulinzi na usalama wa ardhi kwa familia nzima. Bi. Maria na Bi. Paayi walipatiwa ekari kumi (10) kila mmoja kwajili ya kilimo. Wanawake hawa wawili walipata vyeti vya hatimiliki ya kimila mwezi Desemba 2018.

Kwa upande wake Ndugu Yakobo anafarijika kuwa mwanaume wa mfano na kiongozi wa kuigwa na jamii yake na anasema;

> *Mimi kama Mwenyekiti niliyepata mafunzo ya Sheria za Ardhi kuhusu haki za ardhi kwa wanawake nimeamua ni vizuri kuwa dira ili kuwahamasisha wanaume wengine kufanya maamuzi sahihi.*



*Mwenyekiti wa Kijiji cha Orkitikiti Ndugu Yakobo Olisiaji akiwa na wake zake wawili Bi. Maria na Bi. Paayai ambao aliamua kuwapatia ardhi ya kumiliki*



Na Happiness Mfinanga

# NAFASI YA MILA KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI KWENYE ARDHI ZA VIJIJI

Kumekuwa na taarifa nyingi kuhusu migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Migogoro hii ni ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na wakulima na wafugaji, wakulima kwa wakulima, kijiji kwa kijiji, wananchi na wawekezaji, hifadhi za wanyamapori na jamii zinazozunguka hifadhi hizi pamoja na migogoro ndani ya ardhi ndani ya familia na koo.

Baadhi ya vyanzo vya migogoro hii ni pamoja na uelewa mdogo wa sheria za ardhi, mitazamo hasi ya watumiaji wa ardhi, kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi, mila na desturi zinazokandamiza haki za makundi fulani fulani kwenye jamii pamoja na usimamizi ardhi usiozingatia taratibu za kisheria.

Katika utatuzi wa migogoro ya ardhi kumekuwepo na njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na njia za kimila, taratibu za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za mwaka 1999 pamoja na Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ya mwaka 2002. Ingawa kumekuwa na changamoto ya matumizi ya mila katika utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa sababu baadhi ya mila zinawakandamiza wanawake katika kushiriki utatuzi na hata kutendewa haki katika mchakato mzima wa kutatua migogoro hii.

Vilevile matumizi ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata pamoja na yale Wilaya bado ni changamoto katika maeneo mbalimbali kutokana na kutokuwepo kwa mabaraza haya na wajumbe wake kutokuwa na mafunzo ya kutosha ya kuwaongoza katika kutoa maamuzi sahihi wakati wa usuluhishi wa migogoro.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 usimamizi na umiliki wa ardhi ni wa kimila. Hivyo mila zinazokubaliwa na jamii za vijiji husika zinatumika katika usimamizi, umilikishaji na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Lakini pamoja na Sheria kuruhusu matumizi ya mila bado viongozi wa kimila hawakuwa na uelewa wa namna ya kuboresha mila na desturi zao zisikandamize makundi mengine kwenye jamii wanazoziongoza.

Taasisi ya TAWLA kupitia mradi wa "*kukuza upatikanaji wa haki za ardhi na mali kwa wanawake*" unaofadhiliwa na shirika la *Foundation for Civil Society* iliendesha mafunzo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa viongozi wa mila wa kabila la Wameru maarufu kama *"Washili"* katika Wilaya ya Arumeru kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuboresha njia za utatuzi wa migogoro ya ardhi kimila ili kutenda haki.



Wazee wa Kimila wa jamii wa Wameru wakiwa kwenye mafunzo ya utatuzi wa migororo ya ardhi

Baada ya mafunzo haya kwa viongozi hawa wa kimila kumekuwepo na mirejesho ya namna gani mafunzo yalivyosaidia katika kutenda haki wakati wa kusikiliza mashauri haya ya migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuwapa wanawake kipaumbele katika kusikiliza migogoro inayowahusu. Baadhi ya mirejesho hiyo ni kama ifuatayo;

Mshili **Elirehema A. Ayo** wa kata ya Songoro aliyekiliza mgogoro baina ya Bi. Ndelingwa Ndilinyo Sarakikya na Ndugu John Paulo Akyoo, ambao ni mke na mume. Mgogoro ulisababishwa mume kutaka kuuza ng'ombe

wa familia pasipo ridhaa ya mkewe. Mgogoro ulipofika kwa Mshili aliwaita wahusika na kuwasikiliza na uamuzi ulikuwa ni kumshauri na kumuonya mume kuwa hana haki ya kuuza mali ya familia haki kuwepo na makubaliano na mkewe.

Mshili **Lembris Meijo** wa kata ya Kiranyi aliyesikiliza shauri baina ya Bi. Nginyi Tumaini ambae ni mama wa makamo ambaye watoto wa Mama Mkubwa walikuwa wakimnyang'anywa shamba alilopewa na Baba yake wakiamini wao ndio wamiliki halali. Baada ya kufika kwa Mshili walijadiliana walisuluhishwa na shamba kubaki kwenye umiliki wa Bi. Nginyi.

Mshili **Reuben Nanyaro** wa kata ya Poli ambae alitatua mgogoro wa ardhi uliomuhusisha Mama Mafie aliyefiwa na mume wake na ndugu wa marehemu wakataka mama huyo aondoke awaachie ardhi ya ndugu yao. Baada ya kufika kwa Mshili aliwasuluhisha na maamuzi yalikuwa ardhi ni mali halali ya Mjane na watoto wake ambaye alichuma na marehemu mumewe.

Simulizi za Washili hawa zinadhihirisha ni kwa kiasi gani elimu ya Sheria na Haki za Ardhi ni muhimu sana kwa viongozi wa kimila pamoja na jamii kwa ujumla ili mila na desturi zitumike kwa nia njema na sio kunyanyasa kundi fulani na kupendelea jingine.

# WOSIA SIO UCHURO NI ULINZI WA MALI YA FAMILIA



*Na Happiness Mfinanga*

Maana ya wosia ni maandishi au maneno yanayotamkwa na mtu akielezea jinsi mazishi yake yatakavyokuwa, anaweza pia kuelezea mahali atakapozikwa n.k. Vilevile ni agizo atoalo mtu wakati wa uhai wa maisha yake lihusulo namna mali yake itakavyofanywa pindi atakapofariki.

Katika kuandika wosia mhusika lazima azingatie mambo ya muhimu yafuatayo; Mwosia awe na uwezo wa kuandika wosia, yaani asiwe chini ya umri wa miaka 18. Vilevile awe na akili timamu. Kama Mwosia anajua kusoma na kuandika ni lazima kuandika wosia wake mwenyewe. Ni lazima wosia ushuhudiwe na mashahidi wawili na itakapobidi mmojawapo awe mtu wa ukoo wa mwosia. Ikiwa mwosia hajui kusoma na kuandika ni lazima wosia huo ushuhudiwe na watu wanne na wawili kati yao wawe ni watu wa ukoo wa mwosia.

Wosia uandikwe kwa kalamu ya wino au isiyofutika au upigwe chapa. Tarehe ya kuandikwa wosia iandikwe kwa usahihi na uwazi. Wosia utaje kuwa mwosia ametia sahihi yake mbele ya mashahidi wake, wakati mmoja kwa hiari yake mwenyewe na kwamba andiko hilo linashuhudiwa kuwa ni wosia wake ambao utatumika baada ya kifo chake Mwosia asiyejua kusoma au kuandika aelezwe kuhusu wosia wake. Mwosia ataje msimamizi wa mali yake katika wosia. Iwapo mwosia ni mgonjwa wakati wa kuandika wosia, Daktari ahusishwe ili kuthibitisha kuwa mwosia alikuwa katika hali ya kuweza kuandika au kutoa wosia ijapo alikuwa mgonjwa. Warithi hawapaswi kujua Mwosia amewausia nini. Wosia unaweza kuhifadhiwa sehemu yoyote yenye usalama kuepusha uwezo wa kufanyiwa mabadiliko na mtu asiye mwosia. Hivyo sehemu kama vile Benki, Makanisani na Mahakamani n.k. zinafaa kutunzia wosia.

Pamoja na umuhimu wa wosia katika kutunza mali ya familia lakini bado wosia unachukuliwa kama uchuro kwenye jamii nyingi hivyo watu walio wengi hawaandiki wosia mapema. Hivyo kusababisha migogoro mingi pindi mhusika mkubwa wa mali anapofariki pasipokuwa na mwongozo wowote wa namna ya mgawanyo wa mali alizoacha. Mara nyingi waathirika wa migogoro hii wamekuwa ni wanawake na watoto. Kwa mfano katika jamii ya Wameru mwanamke hana haki ya kumiliki mali za Baba wala mume wake pindi anapofariki hata kama walizitafuta wote kwa pamoja.

Vivyo hivyo kwenye familia ambazo zimejaliwa watoto wa kike na kiume, kwenye kurithi mali, watoto wa kiume hupata zaidi ya wa kike. Kwa sababu watoto wa kike huonekana wao wataolewa kwenye familia nyingine hivyo hawastahili

kuwarithi wazazi wao. Lakini majonzi huwa makubwa pale mume anapofariki kwasababu hufukuzwa na wakwe zake na hupoteza haki yake ya kurithi mali na ardhi walizochuma na mumewe. Hivyo kumekuwa na kesi nyingi kuhusu mirathi katika familia mbalimbali ambazo wakati mwingine huchukua muda mrefu kumalizwa hivyo kuwagharimu zaidi wahusika.

Sababu kuu ya watu kutokuandika wosia ni kukosekana kwa uelewa wa uandishi wa wosia na kufungua mirathi kwa taratibu za kisheria. Uandishi wa wosia husaidia kupunguza migogoro ya kuhusu mirathi kwani inampa nafasi mtu kuweza kugawa mali zake atakapokuwa amefariki.

Taasisi ya TAWLA kupitia ufadhili wa shirika la *Foundation for Civil Society* inatekeleza mradi wa *"haki za ardhi wanawake"* katika Wilaya ya Meru, ambapo mojawapo ya mafunzo uandishi na faida ya wosia katika umiliki wa mali ikiwa ni pamoja na ardhi. Mafunzo haya yameibua masuala mengi hasa kwenye ufunguzi wa mashauri ya mirathi ambayo imekuwa ikitatuliwa kwa kutofuata taratibu za kisheria. Kwa kushirikiana na Wasaidizi wa Kisheria, Watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji wanajamii wengi wamepata elimu ya uandishi wa wosia.



*Bi. Felista E. Sarakikya (45) wa kijiji cha Ushili, kata ya Songoro akitoa ushuhuda jinsi Baba mkwe wake ambaye kabla hajafariki aliacha wosia wa kugawanya mali zake kwa watoto wote wa kike na wa kiume. Hii ni faida ya mafunzo ya uandishi wa wosia aliyopata.*

*Mzee Lengaeli A. Mafie "Mshili wa Wameru" ambaye pia ni msaidizi wa kisheria anaetoa huduma za msaada wa kisheria akihamasisha jamii kuhusu uandishi wa wosia.*



*Na Sabina Eugen Ngolahela*

# HAKI ZA ARDHI NI MSINGI WA MAENDELEO KWA WANAWAKE NA JAMII



Maendeleo ni jumla ya maisha ya watu katika jamii pasipo kujali utofauti wa kijinsia kuhusiana na upatikanaji wa elimu, chakula, miundombinu ya usafiri, huduma za afya na uwezo wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na kumiliki mali.

Katika baadhi ya jamii kwenye nchi yetu wanaamini ni wanaume pekee ndiyo wenye uwezo wa kuwa na maendeleo ya kiuchumi na sio wanawake. Kwa jumla mwanamke anachukuliwa kuwa mama wa nyumbani mwenye jukumu la kulea watoto na mume tu. Ndio maana katika maeneo ya vijijini ni wanawake wachache wanamiliki ardhi ambayo ndio nguzo kuu ya maendeleo ya kiuchumi. Hali hii inachochewa na mfumo dume, kukosa kujiamini kutokutambua haki zao za msingi juu ya umiliki, kutumia na kunufaika na ardhi.

Bi. Yusta Gandisa mkazi wa kijiji cha Ilakala wilaya ya Kilosa, Morogoro ni miongoni mwa wanawake ambao walinyanyasika kwa muda mrefu kwa kutokujua haki na wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Bi. Yusta alifiwa na mumewe mwaka 2010 ambaye alikuwa akipambana kupata chakula na kipato kutoka kwenye shamba la ekari mbili (2) ambapo



*Bi. Yusta Gandisa anayeonekana pichani wakati anatoa ushuhuda wake kuwa ni kwa jinsi gani mafunzo ya haki za ardhi yamempa mafanikio ya kiuchumi kupitia kilimo.*




hupata kati ya magunia nane (8) pale msimu unapokuwa mzuri lakini kimsingi haikumtosheleza yeye na familia yake.

Mnamo Februari mwaka 2017 taasisi ya WOPATA inayotekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake unaofadhiliwa na Shirika la *Foundation for Civil Society*. Katika mradi huu kuna mafunzo ambayo yanalenga kuleta hamasa kwa wanawake juu ya kutambua haki zao za msingi juu ya ardhi na maendeleo ya kiuchumi.

Mojawapo ya wanawake walioshiriki mafunzo haya ni Bi. Yusta ambaye hapo awali alikuwa hafahamu kuwa anaweza kupata ardhi zaidi kwajili ya kujikwamua kiuchumi. Baada ya kupata mafunzo, ameweza kuhamasika na kununua shamba mwezi Desemba 2017 ambalo analimiliki yeye mwenyewe na analitumia kuzalisha mazao ya chakula. Kupitia uzalishaji kwenye eneo hilo ameweza kunua vifaa vya shule kwajili ya watoto wake, kununua sola ambayo ameifunga nyumbani kwake.

Mafanikio ya Bi. Yusta yamekuwa ni chachu ya mafanikio kwa wanawake wengine kwenye kijiji anachoishi pamoja na vijana jirani. Hii inaonyesha kuwa ni kwa jinsi gani elimu ya haki za ardhi inaweza kuwa msaada wa kukomboa wanawake wengi ambao hawana ardhi za kilimo na ufugaji.



Na; Neema Samwel Shoo

# UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA ARDHI NI KUFAHAMU HAKI NA WAJIBU WAKE

Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorejelewa mara kwa mara) inaainisha ya kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria. Hivyo wanawake na wanaume wana haki sawa katika kumiliki ardhi kama mojawapo ya mali.

Pamoja na sheria kuruhusu wanawake kumiliki ardhi bado katika jamii kadhaa wanawake hawaruhusiwi kumiliki ardhi bali kuitumia ardhi tu kwa kuzalisha mali aidha kupitia kilimo au ufugaji wala hana maamuzi mengine zaidi ya hiyo ardhi.

Taasisi ya WODSTA kupitia ufadhili wa Shirika la *Foundation for Civil Society* linatekeleza mradi wa kuhamasisha jamii na kuijengea uelewa juu ya umiliki wa ardhi kwa wanawake katika Kata tatu za Wilaya ya Arusha ambazo ni Oldonyosambo, Oldonyowasi na Lengijave.

Baada ya elimu hii mafanikio yameanza kuonekana kwani wanawake wengi pamoja na viongozi wa kimila wamepata uelewa na kubadili mitazamo waliyokuwa nayo kabla ya kupata mafunzo. Kwa mfano Bi. Neema Mungaya wa kijiji cha Lemongo kilichopo katika Kata ya Oldonyosambo ni mmoja kati ya wanufaika.


Bi. Neema ambaye ni mjane aligawiwa ardhi na mume wake kabla ya kufariki na alikua akiitumia ardhi hiyo kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo ili kulisha na kuendesha familia yake lakini mambo yaligeuka baada ya kampuni ya Vodacom kufika kwa ajili ya kutaka eneo litakalofaa kuweka mnara wa mawasiliano. Ndugu wa mume wake walipogundua eneo la mjane huyu linafaa kwa kuwekwa mnara wa simu walianza kumshawishi Mjane akubaliane nao kwa maelezo kwamba fedha zote zitakua mikononi mwake lakini alikataa na hapo ndipo walipoanza visa hadi kumyang'anya eneo lake na kulibadili umiliki na kulitoa kwa Vodacom.

Kampuni ya Vodacom walijenga mnara wakiamini kuna maridhiano baina ya wamiliki wa eneo hilo na walitoa fedha ya fidia ambayo iliishia kwa shemeji zake. Mama huyo aliishi kwa tabu na kuhangaika kwani eneo hilo ndilo alilolitegemea kuzalisha chakula. Pamoja na kupeleka malalamiko sehemu mbalimbali lakini hakupata msaada.

Kupitia mafunzo ya Sheria za Ardhi Mjane huyu alipata nguvu na ujasiri wa kutokata tamaa na kuanza rasmi mchakato wa kufuatilia tena suala hili baada ya kutambua kwamba ilikua ni haki yake na baada ya vikao vya kimila kuonekana kutetea upande mmoja. Aliamua kwenda Mahakama ya Mwanzo iitwayo Emaiyo na hukumu ilitoka kuwa Mjane huyo alipwe fidia na Kampuni ya Vodacom na hasitokee mtu wa kuingilia malipo hayo.



*Huyu ni Bi. Neema ambaye alinyang'anywa ardhi na ndugu wa marehemu mumewe kabla ya kupata elimu ya haki za ardhi na kuikomboa ardhi hiyo.*



*Na Happiness Mfinanga*

# MNYORORO WA UKANDAMIZAJI WA HAKI ZA WANAWAKE WAKATWA NA MSHILI WA WAMERU

Tanzania ni moja ya nchi zenye makabila mengi katika Bara la Afrika. Kabila la Wameru ni moja ya makabila haya linalopatikana Kaskazini mwa nchi katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Meru. Kabila hili ni baadhi ya makabila yaliyofanikiwa kuhifadhi na kutunza mila na desturi zake kwa muda mrefu sasa. Katika kuimarisha na kulinda mila na desturi hizi kabila hili wameandika katiba yenye sheria na kanuni yenye kutoa mwongozo wa namna wanajamii wa kabila hili wanatakiwa kuishi kwa kuheshimu tamaduni zake. Katiba hii inatambulika kama *Katiba ya Wameru*. Halikadhalika, jamii ina viongozi mashuhuri kama *Washili* ambao wanaheshimika ndani na nje ya kabila hili.

Pamoja na kuwa na taratibu nzuri za kusimamia mfumo wa maisha yao bado mila na desturi za kabila hili zinakandamiza haki za ardhi kwa wanawake kwa kiasi kikubwa sana. Wameru kwa asili ni jamii inayojihusisha na kilimo lakini wanawake wanaweza tu kupata ardhi kwajili ya kulima na kuzalisha chakula lakini sio kumiliki.

Hata katika familia ambazo wanafuga wanawake wanaweza kuitunza mifugo lakini akiwa na shida na kutaka kuuza ni lazima apate ruhusa ya Baba yake au mumewe. Katika jamii hii mtoto mdogo wa kiume anapewa mamlaka makubwa ya kumiliki mali kuliko Mama yake mzazi au dada zake.

Baada ya kubaini ukandamizaji huu taasisi ya TAWLA iliamua kutekeleza mradi wa utetezi wa haki za ardhi kwa wanawake katika jamii hii. Njia mojawapo inayotumika na taasisi hii katika kutekeleza mradi huu ni kutoa mafunzo ya Sheria za Ardhi kwa wanaume na viongozi wa kimila wa jamii maarufu kama Washili. Katika kutoa elimu hii kumekuwepo na mafanikio kadha wa kadha ikiwa ni pamoja na wanaume kubadili tabia za mila kandamizi na kuruhusu wanawake kumiliki ardhi.

Kwa mfano, Mzee Rubeni Lesio ambaye aliamua kutoa ardhi kwa binti yake aitwaye Elarusa Reuben na kumruhusu kupata cheti cha hakimiliki ya ardhi ili awe na maamuzi yote juu ya ardhi hiyo. Katika kutekeleza hili Mzee Lesio alichinja mbuzi na kumwaga damu kama ushahidi na agano katika makabidhiano hayo yaliyofanyika mbele ya ndugu zake.

Maamuzi ya Mzee Lesio yamebadili fikra za wanaume wengi kwenye jamii hii ingawa bado kuna wengi wasioamini kuwa mtoto wa kike anaweza kumilikishwa ardhi hata kufikia hatua ya kumlaumu Mzee Lesio ambaye ni Mshili wao na kumuona kama ni msaliti wa mila na desturi zao.




*Taasisi ya HAKIARDHI iliibuka mshindi wa jumla katika maonyesho ya wiki ya AZAKI yaliyoandaliwa na Shirika Foundation For Civil Society Mwezi Oktoba 2018 Dodoma.*

Mradi huu unafadhiliwa na Foundation for Civil Society

THE FOUNDATION for Civil Society